

(IJA)

**CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA LUSHOTO**



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**CHUO KUWAJENGEA UWEZO MAAFISA WAENDESHAJI**

**MASHAURI YA MTOTO MKOANI SUMBAWANGA**

**Tarehe 14/11/2019**

Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) katika programu yake ya kutoa mafunzo kwa maafisa wanaohusika na mashauri ya mtoto kwenye Kanda mbalimbali za Mahakama Kuu watatoa mafunzo kwa maafisa wote wanaohusika katika kuendesha mashauri ya mtoto katika Kanda ya Mahakama Kuu Sumbawanga.

Mafunzo hayo yanatarajiwa kufunguliwa na Jaji Mfawidhi wa Kanda ya Sumbawanga **Mhe. David Eliadi Mrango** mnamo tarehe 18/11/2019 na yanatarajiwa kufikia tamati tarehe 22/11/2019. Licha ya wadau wanaohusika na mashauri ya mtoto kujengewa uwezo wa namna bora ya kuendesha mashauri ya mtoto pia watapata fursa ya kujadili changamoto mbalimbali wanazokutana nazo kwenye uendeshaji wa mashauri hayo na kuweka maazimio yatakayosaidia kuboresha utoaji haki kwa mtoto anayefika mbele ya sheria na anayehitaji ulinzi na usalama.

Mafunzo hayo yanayoendeshwa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania yanafadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia haki ya mtoto (**UNICEF**) na mpaka sasa yamekwisha fanyika katika kanda mbalimbali za Mahakama Kuu ya Tanzania.

Jumla ya washiriki 45 ambao ni Mahakimu, Mwakili wa Serikali, Waendesha Mashtaka, Maafisa Ustawi wa Jamii na Mwakili wa Kujitegemea kutoka mikoa ya Rukwa na Katavi wanatarajiwa kushiriki mafunzo hayo.

Mafunzo hayo yataendeshwa na wakufunzi wabobezi kwenye masuala ya haki ya mtoto kutoka Mahakama ya Tanzania na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

**Imetolewa na Kitengo cha Uhusiano**

Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto

S.L.P. 20

Simu: 255-27-2660133

Barua pepe: [info@ija.ac.tz](mailto:info@ija.ac.tz), [pro@ija.ac.tz](mailto:pro@ija.ac.tz)

Tovuti: [www.ija.ac.tz](http://www.ija.ac.tz)